Upatikanaji wa miti michanga

- Unaweza kuwa na bahati nzuri ya kuwa na kitalu jirani kinachosambaza miche ya miti kwa wingi.
- Pamoja na hayo, wakulima wengi wanotaka kupanda miti mingi wataona ni bora kuotesha miche yao wenyewe. Hii inamaanisha kuwa waweza kuchagua aina ya miti unayohitaji, unaweza kuwa na mbegu au miche tayari wakati utapoihitaji na pia unaweza kujipatia fedha kwa kuuza miche ya ziada kwa wakulima wengine.
- Wakulima wengi wanaacha miti ijiotee yenyewe japokuwa kukuza miti na mazao kwa pamoja, unatakiwa kupanda miti yenye matumizi sahihi unayohitaji, kwa miti mingi ya kienyeji unaweza kukusanya mbegu zake wewe mwenyewe, kwa mbegu za miti ya kigeni waulize wahudumu wa misitu na watafiti ili kuzipata.

Majadiliano F6

- Jadili juu ya upatikanaji wa miche ya miti kwenye eneo lenu. Je kuna kitalu cha miti jirani? Ni aina gani ya miti waliyonayo? Ni rahisi kiasi gani kwa wakulima kupata miche kutoka kwenye kitalu.

- Ni kipindi gani miti mingi ya kienyeji inapotoa mbegu? Kuna urahisi gani kuzikusanya.

- Je wapo washiriki wenye uzoefu wa kukusanya, kutunza na kupanda mbegu za miti?

- Je washiriki wanajua sehemu ambayo mbegu za miti zinakoweza kupatikana? Kwa kawaida kuna vyanzo vizuri katika kila nchi.

Kukusanya na kutunza mbegu za miti

- Jenga tabia ya kutembea na mfuko au bahasha ya zamani ili kila wakati uwe tayari kukusanya mbegu.

- Kusanya mbegu iliyokomaa toka kwenye miti iliyotunzwa vizuri, chukua mbegu toka mifano bora ya miti iliyopo. Mbegu zilizomo kwenye maganda au matunda zatakiwa kutolewa. Kwa matunda ya aina ya vijiti kama mkwaju, mkikwa, mkoga, yanatakiwa kwanza yaliwe au yalowekwe ili mbegu ziweze kutolewa.

- Mbegu ni lazima zikaushwe vizuri kabla ya kutunzwa. Tumia utambulisho sahihi. Baadhi ya mbegu hasa zenye ganda gumu zaweza kukaa kwa miaka mingi bila kuharibika, mbegu laini kama “mwarobaini au mchongoma” zaweza kukaa kwa wiki chache tu. Kila inapowezekana tumia mbegu mpya.

Majadiliano F7

- Ni tabia gani za mbegu nzuri za miti? Hii itategemea sababu za watu wanaolima miti kwa mfano mti wenye matunda mazuri utatoa mti mzuri wa matunda na mti mrefu ulionyoka utatoa mbao nzuri.

- Mjadili ni vyombo gani vilivyopo vinavyoweza kuwa vya kufaa kwa kutunzia mbegu. Vinatakiwa kuwa safi, vikavu vyenye uwezo wa kutoa hewa nje na unyevunyevu. Kwa mawazo mengine vifaa hivyo vinaweza kuwa majagi, makopo, vyombo vya plastiki, mifuko ya plastiki au vibuyu.

- Kama kikundi, andaeni vyombo vya kufaa na vitambulisho. Halafu, kama inawezekana mwende kukusanya baadhi za mbegu. Mnaweza kufanya hivi kwa vipindi fulani vya mwaka kwa jamii nyingi ya miti. Ruhusu mbegu kukauka vizuri kabla ya kuweka ndani ya vyombo.

- Je ni vyanzo gani vya mbegu washiriki wanavyo vifahamu? Hivi vinaweza kuhusisha idara ya misitu, Wizara ya Kilimo na Mashirika yasiyo ya kiserikali ya wenyeji NGO's. Kama hamuwezi kupata mbegu katika nchi yenu kwa ajili ya miti mnayotaka, baadhi ya mbegu kidogo inaweza kupatikana kutoka:

  ECHO – 17391 Durrance Road, North Fort Myers FL 33917 USA
  E-mail:ech@echonet.org Fax: +941 543 5317

  HDRA – Centre for Organic Gardening, Ryton on Dunsmore, Coventry, CV8, 3LG, UK.

Upandaji wa mbegu za miti moja kwa moja

- Miti mingi inaweza kupandwa moja kwa moja ardhini, panda mistari ya mbegu kwa kufuata sura ya nchi au kuzunguka nje kidogo ya shamba.

- Panda mbegu aidha kabla ya mvua kuanza au mapema katika msimu wa mvua, kama kutakuwa na uhaba wa mvua itabidi kumwagilia miche mara moja au mbili ukiwezekana kwa siku.



- Baadhi ya miti inaweza kukuzwa kwa kutumia vitawi au vishina. Kata vipande vya miti ya mgrilisidia, mlonge, mkalianda katika vipingili. Toa majani yote vipingili hivyo vinaweza kuwa na urefu wa cm 30 – 40cm na kupandwa kwa kuinamisha upande, (pembe) au waweza kukata vipande vya mita mbili na kupanda wima ili vichipukizi visifikiwe na wanyama waharibifu.



Majadiliano F8

- Nini faida ya kupanda mbegu moja moja shambani ukilinganisha na kazi ya kutengeneza kitalu.
- Kuna mshiriki yeyote mwenye uzoefu wa kupanda miti moja kwa moja kwa mbegu? Je ni aina gani ya miti inayofaa kupandwa moja kwa moja?
- Kuna mshiriki yeyote ana uzoefu wa kupanda miti kwa kutumia kitawi au shina? Ni aina gani ya miti iliyoonyesha mafanikio na ilifanyika namna gani?
- Kama kuna uwezekano tembelea mkulima ambaye tayari amepanda miti na mazao mengine kwa mstari ili kujifunza kutokana na uzoefu wao.
- Andaa muda mzuri wa kwenda kupanda mistari kadhaa ya miti kwenye shamba la mmoja wa washiriki au baadhi yao.

Kuandaa kitalu cha miti

- Ni rahisi kujenga na kutunza kitalu cha miti. Hii inawezekana kuanza miti michache unayoweza kuotesha kwenye kivuli karibu na nyumbani na kitalu kikubwa chenye mamia ya miche michanga.

- Kitalu kikubwa cha miti lazima kiwe karibu na chanzo cha maji cha kudumu, katika eneo la tambarare ambalo haliwezi kupata mafuriko wakati wa masika (mvua). Udongo lazima uwe na rutuba kusiwe na mifugo inayozurura karibu na kitalu.

- Kwa kitalu kidogo ni bora kuwa nacho karibu na nyumbani ili miti midogo iweze kulindwa na uharibifu wa wanyama na wezi.

- Kama hakuna miti mikubwa ya kutoa kivuli, utahitaji kujenga kivuli.

Majadiliano F9

- Tembelea kitalu kizuri cha miti, kama inawezekana tembelea kitalu kikubwa na kitalu kidogo.

- Jadili kuhusu uzoefu wa mkulima mwenyeji aliyejenga kitalu cha miti.

- Wahimize washiriki kufikiri juu ya miti itakayofaa kwa kivuli karibu na nyumba zao ambapo wataweza kuotesha miche michache. Na wanaweza kuilinda vipi isiharibiwe na kuku, mbuzi, na mifugo mingine.

- Jadili tofauti za sehemu na asili inayohitajika katika kuotesha miche kwenye matuta, kutokana na mahitaji hayo kama miche itaoteshwa kwenye vyungu au vifuko, je aina ya udongo ni muhimu?

- Jadili eneo la karibu linaloweza kufaa kwa kundi la wakulima wa kufungua vitalu vikubwa vya miti.

Vyombo vinavyofaa kwa mbegu za miti

- Mbegu zinaweza kupandwa kwenye aina zote za vyombo vya mirija ya plastiki, makasha ya maziwa, mifuko ya plastiki, makopo au vyungu zilivyovunjika. Vyombo vyote hivyo lazima viwe na matundu kwenye kitako ili maji yaweze kutiririka.

- Mbegu zinaweza pia kupandwa kwenye matuta, tengeneza tuta lenye upana wa sm60 na urefu wa kutosha unaohitajika. Tumia mbao, nguzo au nguzo za katani, kama unazo mbao za kutosha unaweza ukatengeneza masanduku madogo yanayohamishika yenye ukubwa wa sm40 x sm40 yenye kitako, mbao zako zipake oil iliyotumika.

- Tumia udongo mzuri wa rutuba kujaza kwa vyombo hivyo na kwenye matuta, kama inawezekana udongo huo utoke chini ya miti kwa kuwa udongo huo utakuwa na vijidudu (organism) vinavyosaidia ukuaji wa mizizi ya miti, changanya sehemu 4 ya udongo mzuri na sehemu 2 ya mchanga wa mtoni na sehemu 1 ya mbolea kavu. Changanya pamoja vyote vikiwa vikavu. Jaza udongo kwenye vyombo kwa uangalifu na tingisha ili ujishindilie vizuri.



Majadiliano F10

- Ni aina gani ya vyombo vinavyoweza kutumika kupandia mbegu miti? Unaweza kufikiria juu ya vyombo vya plastiki vya misitu kutoka kwa watengenezaji wa karibu? Au chimbuko la vifuko vya plastiki.
- Ni wapi kwenye asili nzuri ya mchanga mzuri na mbolea ya asili?
- Je mnaweza kufanya kazi pamoja kutayarisha vyombo vya kupandia?
- Ni wakati gani mzuri kupanda mbegu za miti ili miche iwe tayari mapema wakati wa mvua kwa kupandikizwa?

Upandaji mbegu

- Panga upandaji ili miche ya miti iwe tayari wakati wa masika. Miche mingi ya miti inahitaji muda wa miezi 4 hadi 6 kwenye kitalu cha miti kabla ya kupandwa shambani.

- Panda mbegu mbili au tatu katika kila chombo. Mbegu nyingine za miti zina ganda gumu zinahitaji msaada ili ziweze kuota na kukua, kwa mfano mlusina, mwati, zitatakiwa zilowekwe kwenye maji ya moto (siyo yanayochemka) usiku kucha kusaidia kuotesha. Au unaweza kutumia msasa au kisu chenye ncha kali kukata kidogo ganda la mbegu.

- Kama unapanda kwenye tuta panda mbegu kwa mstari labda kama mbegu hizo ni ndogo sana kuzimudu, changanya hizo mbegu ndogondogo na mchanga laini kabla ya kuzitawanya. Fukia mbegu na udongo laini.



Majadiliano F11

- Je kupanda mbegu mbili au tatu ni uharibifu?

- Kuna baadhi ya mbegu za miti zimetengenezwa kusudi ziweze kuota baada ya misitu kuungua. Ni kwa namna gani kwa matumizi ya moja ya moto yanasaidia kufuatisha joto la moto?

- Mbegu zenye ganda gumu huchukua muda wa miezi mingi kuota, labda zilowekwe kwenye maji ya moto au kusuguliwa na msasa ili kulainisha ganda hilo gumu. Jadili ni jnsi gani wawezqa kufanya jaribio ili upate njia bora zaidi.

- Ni aina gani za mbegu za miti ya kienyeji zitatakiwa kutendewa namna maalum?

- Kama inawezekana kukusanya aina mbalimbali za mbegu za miti nafikiria kila mbegu inavyohitajika kutendwa kabla ya kuotesha.

- Je unacho chombo cha kumwagilia? Kama huna unaweza kutengeneza chombo cha kumwagilia kutokana na buyu kama ilivyoonyeshwa kwenye mchoro au toboa matundu kwenye kitao cha kopo au chupa ya plastiki.